



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu. 03-3425-4531 FAX. 03-3425-7844
Barua pepe: tzrepjp@tanzaniaembassy.or.jp
tokyo@nje.go.tz

UBALOZI WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA
21-9, KAMIYOGA 4-CHOME.
SETAGAYA-KU, TOKYO 158-0098

FURSA YA MASOMO NA UFADHILI WA PROGRAMU YA UTOKYO COLLEGE OF DESIGN

Ubalozi wa Tanzania nchini Japan unapenda kuwajulisha Watanzania kuhusu fursa ya masomo katika Chuo Kikuu cha Tokyo (The University of Tokyo) kupitia UTokyo College of Design.

1. Kuhusu Programu

Programu hii ni ya miaka 5, inayojumuisha Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili katika programu moja endelevu. Masomo yote yanafundishwa kwa Kiingereza. Programu inajumuisha taaluma mtambuka zinazohusu ubunifu, teknolojia, sayansi, jamii na mazingira, kwa lengo la kutumia fikra bunifu katika kutatua changamoto za kiuchumi na kijamii. Masomo yanatarajiwa kuanza Septemba 2027.

2. Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe amehitimu na kufaulu Kidato cha Sita au Diploma inayotambuliwa na Chuo Kikuu cha Tokyo, pamoja na kukidhi masharti mengine ya kitaaluma na lugha ya Kiingereza.

3. Njia za Udahili

Route A: Kwa waombaji wanaoishi nchini Japan ambao watatakiwa kufanya Common Test for University Admissions ya Japan. Usaili wa hatua ya pili utafanyika ana kwa ana nchini Japan.

Route B: Kwa waombaji wanaoishi nje ya Japan ambao wamehitimu na kufaulu Kidato cha Sita au Diploma inayotambuliwa na Chuo Kikuu cha Tokyo, pamoja na kukidhi masharti mengine ya udahili. Usaili utafanyika kwa njia ya mtandao kwa lugha ya Kiingereza.

4. Fursa za Ufadhili

- Needs-Based Scholarship: Hutoa msaada wa kugharamia ada ya kujiunga, ada za masomo, gharama za maisha nchini Japan na nauli ya ndege kwenda Japan kwa wanafunzi wanaoishi nje ya Japan.
- Merit-Based Scholarship: Hutolewa kwa wanafunzi wenye ufaulu bora wa kitaaluma ili kusaidia gharama za masomo.

5. Muda wa Maombi

Maombi yataanza kupokelewa tarehe 15 Oktoba 2026 saa 3:00 asubuhi kwa saa za Japan (JST), sawa na saa 9:00 alasiri kwa saa za Tanzania. Muda wa mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 5 Novemba 2026 saa 11:00 jioni kwa saa za Japan (JST), sawa na saa 5:00 asubuhi kwa saa za Tanzania.

6. Namna ya Kutuma Maombi

Maombi ya udahili yanafanyika kwa njia ya mtandao kupitia tovuti rasmi ya Chuo Kikuu cha Tokyo. Waombaji wanashauriwa kusoma kwa makini masharti rasmi ya udahili kabla ya kutuma maombi.

Kiungo rasmi cha maombi: <https://design.adm.u-tokyo.ac.jp/admissions/application-guidelines-2027/>

**Ubalozi wa Tanzania nchini Japan unawahimiza Watanzania wenye sifa
kuchangamkia fursa hii**

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NCHINI JAPAN

09 OKTOBA, 2026